JARIDA LA TFF

MWEZI OKTOBA, 2026







YALIYOMO


UJUMBE KUTOKA KWA RAIS 3


SARAFU YAIONDOA SERENGETI BOYS AFCON 2027 5


SIMBA QUEENS WABABE NGAO YA JAMII 2026 6


TWIGA STARS KUWAKABILI ETHIOPIA OLIMPIKI 8


UWANJA WA UHURU 9


YOUNG AFRICANS YAWEKA HISTORIA CAFCL 2026/27 10



LIGI KUU YA NBC YAWEKA REKODI YA FVS 11


SIMBA YAANDIKA REKODI MAKUNDI CAFCL 2026/27 12


AZAM FC, SINGIDA BS ZATINGA TENA MAKUNDI CAF 14

MAELEZO YA UCHAPAJI

Jarida hili huchapishwa kila Mwezi
na Shirikisho la Mpira wa Miguu
Tanzania (TFF)

Mhariri Mkuu:
Evans Mgeusa

Mhariri Habari:
Cliford Mario Ndimbo

Mhariri Msaidizi:
Erasto Masalu

Meneja Masoko:
Aaron Nyanda

Msanifu Kurasa:
Gabriel Johnson

Mpiga Picha:
Innocent Okama

Wachangiaji:
Zaituni Yusuph, Musa Mateja, Cosmas Komba, Tusekile Frank

Tuwaunge mkono Serengeti Boys Kombe la Dunia Qatar



Tumekuwa tukipambana sana kuhakikisha Timu zetu za Taifa zinafanya vizuri na kushiriki kwenye mashindano mbalimbali na kufanya vizuri, tuliamua kuwekeza kuanzia chini kwa lengo la kuibua na kuendeleza vipaji huku tukitazama ushiriki wetu katika mashindano tofauti.

Uwekezaji huo sio rahisi, tulidhamiria na sasa tumeanza kuona matunda ya uwekezaji wetu kuanzia kwenye ngazi ya chini kwa timu zetu kuanza kushiriki na kufanya vizuri kwenye mashindano makubwa.

Timu zetu zimefanikiwa kucheza katika mashindano mbalimbali ikiwemo AFCON na Kombe la Dunia ambako itakumbukwa Timu yetu ya taifa U17 Serengeti Girls walifungua mlango baada ya kufuzu Kombe la Dunia kwa wasichana U17 zilizofanyika nchini India 2022, lakini pia Wanawake U20 Tanzanite Queens nao walifanikiwa kufuzu fainali za Kombe la Dunia 2026 Poland na sasa ni kwa upande wa Wavulana U17 Serengeti Boys ambao wanakwenda kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa wavulana U17 zitakazofanyika nchini Qatar kuanzia Novemba 19 mpaka Desemba 13, 2026.

Kama ilivyokuwa kwa Serengeti Girls ilipoweka historia iliyodhihirisha uwezo wetu wa soka unavyozidi kukua na kuwa timu ya kwanza ya Tanzania ya wanawake kufuzu Kombe la Dunia, ndivyo hivyo ilivyo kwa Serengeti Boys ambayo nayo imeweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza ya Tanzania kwa wanaume kufuzu Kombe la Dunia.

Hatua ambayo timu yetu ya Serengeti Boys imepiga kwenye ramani ya soka la Afrika inaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa timu 10 kutoka Afrika zinazoshiriki fainali hizo ikiwa pamoja na Cameroon, Misri, Ivory Coast, Morocco, Algeria, Mali, Senegal, Msumbiji na Uganda.

Kwetu sisi wanafamilia wa mpira wa miguu tunafarijika kufika moja kati ya hatua kubwa kwa mara nyingine baada ya kufanikiwa kwa timu ya wasichana, ambapo tulitamani kuona timu ya wanaume nayo inafuata nyayo hizo na hatimaye Serengeti Boys imefanikisha hilo.

Serengeti Boys kwa sasa wapo katika maandalizi kuelekea katika fainali hizo ambazo wamepangwa Kundi I pamoja na timu za Brazil, Republic of Ireland, na Costa Rica.

Kwa upande wetu TFF kwa kushirikiana na Serikali chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tumeendelea kushirikiana kwa karibu kuhakikisha kuwa wachezaji wanapata maandalizi mazuri ili waweze kutimiza majukumu yao uwanjani na kufanya vizuri na kuweka historia katika mashindano hayo makubwa.

Tunaendelea kuwaomba Watanzania kuwaunga mkono wakati wote ambao watakuwa wakipeperusha bendera ya Tanzania huko Qatar.

Serengeti Boys wanabeba matumaini makubwa ya Watanzania kwenye mashindano hayo, hivyo ni jukumu la kila mtanzania kwa nafasi yake kuwaunga mkono kwa namna yoyote katika kila mechi watakayocheza kwenye michuano hiyo.

Vijana wetu wa Serengeti Boys wataanza kuipeperusha bendera ya Tanzania Novemba 21, 2026, kwa kucheza na Costa Rica, mechi ya pili itakuwa dhidi ya Brazil itakayochezwa Novemba 24, 2026 na mechi ya mwisho ya hatua ya makundi itachezwa Novemba 27, 2026 dhidi ya Republic of Ireland.

Kwa umoja wetu huu ni muda sahihi kila Mtanzania kuisapoti Serengeti Boys katika mechi hizo tatu za kwanza ili waweze kufuzu hatua inayofuata kama sehemu muhimu ya kuweka rekodi nyingine ambayo itatutangaza zaidi katika ulimwengu wa soka.

WALLACE KARIA
RAIS WA TFF

NetFlix Show Show

NBC
Benki ya Taifa ya Biashara
Daima Karibu Nawe.

Kamilisha malipo ya Subscription kwa **NBC VISA Debit Card** ule mamuvi bila makato ya ziada



#NBCDaimaKaribuNawe



Sarafu yaiondoa Serengeti Boys AFCON 2027

Timu ya Taifa ya Wavulana U17 (Serengeti Boys) imeondolewa katika michuano ya kufuzu AFCON 2027 Kanda ya CECAFA kwa kurusha sarafu baada ya kufanana katika maeneo yote na Somalia.

Serengeti Boys na Somalia zote zilikusanya pointi 4 katika mechi mbili walizocheza wakishinda kwa mabao 2-0 walipocheza na Kenya na mchezo uliowakutanisha wenyewe kumalizika kwa sare ya bao 1-1 na kufanya timu hizo kufanana kila kitu hivyo ili kupata timu moja ya kuingia nusu fainali ikalazimika kurushwa sarafu kwa mujibu wa kanuni.

Kwa mujibu wa kanuni ya 13 (c) ya CAF, inaeleza kuwa endapo timu zaidi ya mbili zitakuwa zimefanana mwishoni mwa mechi za hatua ya makundi na kufungana kwa kila kitu, uamuzi utafanyika kwa kupiga kura ya bahati nasibu, utakaofanywa na Kamati ya Maandalizi.

Baada ya maamuzi hayo ya kuruşha sarafu, Somalia ilifuzu hatua ya nusu fainali kwa kuongoza Kundi C baada ya sarafu kuangukia upande wake, akiungana na Uganda iliyoongoza Kundi B na Rwanda walioongoza Kundi A wakati Ethiopia akifuzu kupitia mshindi wa pili mwenye matokeo mazuri (Best looser).



SIMBA QUEENS WABABE NGAO YA JAMII 2026



Timu ya Simba Queens imeibuka washindi wa Ngao ya Jamii Wanawake baada ya kuichapa JKT Queens kwa bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa Oktoba 3, 2026, kwenye Uwanja wa KMC, Mwenge jijini Dar es Salaam.

Aisha Mnunka ndiye aliyeamua fainali hiyo kwa bao lake pekee la kipindi cha pili.

JKT Queens waliibuka kuwa washindi wa pili wakati Yanga Princess wenyewe waliibuka washindi wa tatu baada ya kuichapa Mashujaa Queens kwa mikwaju ya penati 5-4, baada ya dakika 90 kumalizika kwa sare ya bao 1-1.







Twiga Stars kuwakabili Ethiopia Olimpiki

Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), itacheza na Ethiopia kwenye raundi ya tatu ya kuwania kufuzu Olimpiki itakayofanyika Los Angeles, Marekani 2028.

Twiga Stars imefuzu raundi ya tatu kwa kishindo baada ya kuifunga Botswana kwa jumla ya mabao 7-0 katika mechi mbili za nyumbani na ugenini, katika mchezo wa kwanza wakishinda kwa bao 1-0 na mechi ya marudiano wakiwachapa mabao 6-0.

Mechi za raundi ya tatu zimepangwa kuchezwa kati ya Februari 23 hadi Machi 6, 2027.

Mashindano ya Olimpiki Los Angeles 2028 yanatoa nafasi kwa timu mbili kutoka Afrika kufuzu.

azamtv

LIGI ZOTE vizi 28,000 tu!

BUNDESLIGA

LALIGA

SERIE A

DFB-POKAL



sisi ni soka!

FKF PREMIER LEAGUE

NBC PREMIER LEAGUE

AFL AFRICAN FOOTBALL LEAGUE

MECHI KALI NA BURUDANI ZAIDI!





Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam utatumiwa na Klabu za Tanzania Simba SC, Young Africans, Azam FC na Singida BS zilizofuzu hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFCL) na Kombe la Shirikisho Afrika (CAFCC).

Young Africans yaweka historia makundi CAFCL 2026/27



Klabu ya Young Africans imeweka historia ya kutinga katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFCL) kwa mara nne mfululizo baada ya kuiondoa CFFA ya Madagascar kwa jumla ya mabao 8-1.

Young Africans imeingia katika hatua hiyo baada ya kuibuka na ushindi katika mechi ya pili ya marudiano dhidi ya CFFA kwa mabao 4-1, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam Oktoba 21, 2026.

Katika mechi ya kwanza ambayo pia ilichezwa katika uwanja huo kutokana na CFFA kutokuwa na uwanja uliokidhi viwango vya CAF, walipoteza kwa mabao 4-0, Oktoba 17, 2026.

Kutinga makundi katika msimu huu inakuwa mara ya nne mfululizo kwa Young Africans kuanzia msimu wa 2023/24, 2024/25, 2025/26 na sasa 2026/27

Young Africans ilitinga katika raundi ya pili baada ya kuiondoa Gaborone ya Botswana kwa jumla ya mabao 3-2, katika mechi ya kwanza iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1 jijini Gaborone na waliporudiana Dar es Salaam walishinda kwa mabao 2-1.

Hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika inatarajiwa kuanza kutimua vumbi kuanzia Novemba 27, 2026 na kumalizika Januari 24, 2027.



Ligi Kuu ya NBC yaweka rekodi ya FVS

Ligi Kuu ya NBC imeweka rekodi ya kuwa ligi ya kwanza duniani kutumia teknolojia ya FVS (Football Video Support) kuwasaidia Waamuzi kwenye maamuzi, baada ya Shirikisho la Mpira la Kimataifa (FIFA) kuruhusu mfumo huo kutumika.

Fifa wamewahi kutumia kwa majaribio teknolojia hiyo katika baadhi ya mashindano tofauti na ligi ya NBC ambayo imeruhusiwa kutumia teknolojia hiyo ikiwa kama ligi ya mfano duniani.

Teknolojia ya FVS imeanza kutumika rasmi Oktoba 8, 2026 ambapo mechi zote 240 zitatumia teknolojia hiyo, na mechi 150 kati ya hizo ripoti zake zitawasilishwa Fifa, ili kuwapa nafasi ligi nyingine duniani kujifunza kutoka Tanzania.

Fifa iliwahi kutumia teknolojia ya FVS katika mashindano mengine kama sehemu ya majaribio ikiwemo Kombe la Dunia la Wanawake U20 lililofanyika nchini Colombia 2024.

Pia ilitumika katika Kombe la Dunia la Wanawake U17 lililofanyika Jamhuri ya Dominika 2024, Kombe la Dunia la Wanaume U20 Chile 2025 na Kombe la Dunia la Wanaume U17 Qatar 2025.

Teknolojia ya FVS imeanzishwa na Fifa ikiwa na lengo la kutumika kama teknolojia mbadala ya VAR (Video Assistance Referee).

Simba yaandika rekodi Makundi CAFCL 2026/27



Klabu ya Simba imekuwa timu pekee iliyofuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFCL) 2026/2027 ikiwa na idadi kubwa ya mabao ya kufunga kuliko timu nyingine zote zilizofuzu katika hatua hiyo, wakifunga jumla ya mabao tisa.

Simba imefuzu hatua ya makundi wakiiondoa 15 de Agosto ya Equatorial Guinea kwa jumla ya mabao 9-1 ambayo yalipatikana katika mechi mbili walizocheza ugenini na nyumbani, wakishinda ugenini kwa mabao 6-1 na mechi ya nyumbani wakashinda kwa mabao 3-0.

Katika hatua ya awali raundi ya kwanza na raundi ya pili, Simba imefunga jumla ya mabao 16 na kuruhusu nyavu zao kutikiswa mara mbili baada ya kuichapa Mighty Wanderers ya Malawi kwa jumla ya mabao 7-1 kwenye raundi ya kwanza ya hatua ya awali, ambapo walishinda ugenini Blantyre, Malawi kwa bao 1-0 kabla ya kufunga mabao 6-1 katika mechi ya marudiano iliyochezwa uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na mechi ya raundi ya pili dhidi ya 15 de Agosto wakishinda 6-1 mechi ya mkondo wa kwanza na kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 mechi ya mkondo wa pili.

Rani
Sanitary Pads

RANI INVESTMENTS LIMITED



Rani Pads



Rani Baby Royal Wipes



Rani Maternity Pads



Rani Pant-liners



Rani Baby Bottle

0754 311 616
ranisanitarypads
raniinvestmentsltd@gmail.com

RANI INVESTMENTS TZ LIMITED
Located at Kinondoni Mwananyamala "A"
Plot 1, Block 35A
P.O.BOX 1002 Dar es salaam

Azam FC, Singida BS zatinga tena Makundi CAF

Klabu za Azam FC na Singida BS zimetinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAFCC) ikiwa ni mara ya pili mfululizo baada ya kutinga hatua hiyo msimu uliopita kwa mara ya kwanza.

Azam FC imetinga hatua hiyo baada ya kuitupa nje ZED ya Misri kwa jumla ya mabao 2-1,mechi ya kwanza ya raundi ya pili ya hatua ya awali wakitoka sare ya bao 1-1 ugenini na katika mechi ya marudiano wakicheza nyumbani wakaibuka na ushindi wa bao 1-0.

Singida BS yenyewe imefuzu baada ya kuichapa Tusker ya Kenya kwa jumla ya mabao 2-1, mechi ya kwanza wakishinda kwa bao 1-0, Nairobi, kabla ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani.

Azam FC na Singida BS zilifuzu kwa mara ya kwanza katika hatua hiyo ya makundi msimu uliopita.





FVS yaanza kutumika Ligi Kuu ya NBC



Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Kuu (TPLB), Cornel Barnabas amesema Mfumo wa Football Video Support (FVS) sasa unaanza kutumika katika mechi zote 240 za Ligi Kuu ya NBC, baada ya kupata ruhusa ramsi kutoka kwa Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA).

Amesema baada ya kukamilisha taratibu zote zilizotakiwa kwa mwongozo wa Fifa, sasa FVS inatumika rasmi ambako itaendana na kutoa ripoti kwa FIFA ili iwe sehemu ya kujifunza kwa nchi nyingine ambazo hazijaanza matumizi ya FVS.

Alisema FVS imeanza kutumika Oktoba 8, 2026 ambapo mechi 150 kati ya 240 ndizo zitakazotolewa ripoti Fifa, ili kuwapa nafasi ligi nyingine duniani zenye lengo la kutumia mfumo huo waweze kujifunza kutoka Tanzania.

Kila timu inapata kadi mbili za kuomba mapitio ya tukio ndani ya sekunde 60 baada ya kutokea.

Serengeti Boys Yapiga hesabu Kombe la Dunia Qatar 2026

Timu ya Taifa ya Wavulana U17 (Serengeti Boys) inaendelea kupiga hesabu zake kwenye maandalizi ya fainali za Kombe la Dunia 2026 zinazotarajiwa kufanyika nchini Qatar kuanzia Novemba 19 mpaka Desemba 13, 2026.

Serengeti Boys ambayo imekuwa timu ya kwanza ya Tanzania kwa wanaume kucheza Kombe la Dunia, imekaa kambini takribani miezi miwili, huku ikifanikiwa kushiriki mashindano mbalimbali kama sehemu ya maandalizi ya michuano hiyo.

Kikosi hicho kilichopangwa katika Kundi I na timu za Brazil, Republic of Ireland pamoja na Costa Rica, ilipata nafasi ya kushiriki michuano ya CFA iliyofanyika katika mji wa Yinchuan nchini China iliyoanza Julai 5-11, 2026 ambako ilicheza na Australia, Nigeria na China.

Katika michuano hiyo Serengeti Boys ilifanikiwa kushinda dhidi ya Nigeria mabao 3-2, ikawafunga wenyeji China mabao 2-0, na mechi ya mwisho ikiichapa Australia kwa mabao 5-3.

Serengeti Boys pia ilishiriki kwenye mashindano ya Veltex Cup yaliyofanyika jijini London Uingereza kama sehemu ya maandalizi ikicheza mechi tatu dhidi ya China, Argentina na Mexico.

Katika michuano hiyo Serengeti Boys walishinda 1-0 dhidi ya China, wakapoteza dhidi ya Argentina kwa mabao 3-2 na mechi ya mwisho wakafungwa na Mexico kwa mabao 3-1.

Mashindano mengine ambayo Serengeti Boys ilipata nafasi ya kushiriki ni yale ya huko Korea Kusini wakicheza mechi tatu dhidi ya Yeosu Marine U18 Football Club, Suwon Samsung Bluewings U18 na Busan IPARK U18.

Serengeti Boys wataanza kuipeperusha bendera ya Tanzania katika michuano ya Kombe la Dunia Novemba 21, 2026 watakapocheza na Costa Rica wakati mechi ya pili itakuwa dhidi ya Brazil ikayochezwa Novemba 24, 2026 na mechi ya mwisho katika hatua ya makundi itachezwa Novemba 27, 2026 dhidi ya Republic of Ireland.



Rais Karia azipongeza Klabu za Tanzania kufuzu makundi CAFCL, CAFCC 2026/2027

Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia amezipongeza timu za Simba SC, Young Africans, Azam FC na Singida BS kwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFCL) na Kombe la Shirikisho Afrika (CAFCC).

Rais Karia amezipongeza timu hizo akisema ni hatua ya kujivunia kwa Tanzania kupeleka timu nne kwenye hatua ya makundi ikiwa ni kwa mara ya pili mfululizo baada ya kufanya hivyo kwa mara ya kwanza msimu uliopita 2025/2026.

Ameongeza kuwa, Tanzania ni moja kati ya mataifa mawili yaliyoingiza timu nne kwenye CAFCL na CAFCC huku akijivunia hatua hiyo akisema inaongeza nguvu ya kufanya vizuri zaidi kama Nchi ikizingatiwa kuwa Morocco wenye miundo mbinu bora zaidi Afrika ndio nchi nyingine iliyoweza kupeleka timu nne kwenye hatua hiyo ya makundi.



Rais wa TFF, Wallace Karia alipokutana na viongozi wa Klabu za Simba SC, Young Africans, Azam FC na Singida BS zilizofuzu hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFCL) na Kombe la Shirikisho Afrika (CAFCC), kwenye kikao cha mkakati na ziara ya kutembelea miundombinu ya uwanja wa Uhuru, wengine walioshiriki ni Katibu Mkuu wa TFF, Evans Mgeusa, viongozi wengine wa TFF na Wawakilishi wa Serikali wanaosimamia uwanja wa Uhuru na Benjamin Mkapa.





Unforgettable Travels Await







Enjoy convenient and reliable flights to Iringa with Precision Air

Precision Air is Now Flying to Iringa

Experience the charm of Iringa with our new flights! Enjoy affordable fares starting from just **99,000 TSH** one-way and **190,000 TSH** round-trip.

- Convenient flight schedules
- Comfortable and reliable service
- Affordable fares for a seamless journey

Scan to book your ticket today and explore Iringa hassle-free!

You are why we fly

Precision Air



Tanzania U15 yaweka alama Kombe la Dunia Azerbaijan

Timu ya Taifa ya Wavulana U15 imeweka alama na kujivunia ushiriki wake wa mara ya kwanza katika michuano ya Kombe la Dunia iliyofanyika Baku, Azerbaijan.

Katika michuano hiyo Tanzania ilicheza mechi 11 ambapo kati ya hizo walifanikiwa kuibuka na ushindi katika mechi sita, kupoteza nne na ikitoka sare moja.

Tanzania katika mechi hizo 11 walizocheza ambazo 10 zilikuwa za mashindano moja ikiwa ya kirafiki walifanikiwa kufunga jumla ya mabao 34 na kuruhusu mabao 14 pekee.

Michuano hiyo ambayo ilichezwa katika mfumo wa makundi, Tanzania ilipangwa Kundi X ikiwa na timu za Zambia, Uruguay, Comoros, Moldova na Montenegro na ilimaliza nafasi ya nne katika msimamo.

TABASAMU KAMBI POPOTE

Tuma pesa, pokea pesa
na kulipa bili msimu huu
wa sikukuu kupitia **SimBanking,**
TemboCard, ATM, Lipa Hapa,
CRDB Wakala na Internet Banking



WAKALA

ATM

Simbanking

Lipa Hapa

CRDB BANK


JUSTFIT
Sports Gear
MUSAHI
JUSTFIT
Gear
JUSTFIT
MORE THAN A STORE,
WE'RE YOUR
FITNESS
PARTNER!
100% AUTHENTIC
PREMIUM QUALITY
EXPERT ADVICE
THANK YOU FOR TRUSTING JUSTFIT SPORTS GEAR STORES.
VISIT US AT:
Mlimani City Mall - Dar
Oilcom Kijitonyama - Dar
Oilcom Mbezi - Dar
AIM Mall - Arusha
Kunduchi Mall - Dar
Chole Rd - Masaki, Dar



Bonyeza Link:
http://mixlr.com/tffonlineradio



Karume Memorial Stadium/Shaurimoyo Road
P.O.Box 1574, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone: +255 22 2182032 Fax: +255 22 2182031
Email: tanfootball@tff.or.tz Website: www.tff.or.tz